

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA ISHIRINI NA MBILI

07 MEI, 2019



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA ISHIRINI NA MBILI – TAREHE 07 MEI, 2019

### I. DUA:

### II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,  
JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha, 2019/2020.

### **MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha, 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2019/2020.

## **MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2019/2020.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

#### **176. MHESHIMIWA SHAABANI OMARI SHEKILINDI (LUSHOTO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Hospitali ya Wilaya ya Lushoto ni ya muda mrefu na hata ujenzi wa majengo yake ni wa kizamani ambao hauendani na utoaji huduma na Serikali ina utaratibu wa kukarabati na kuongeza majengo katika Hospitali za Wilaya:-

Je, ni lini Hospitali ya Wilaya ya Lushoto itakarabatiwa.

## **177. MHESHIMIWA ZUBEDA HASANI SAKURU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Hospitali na Vituo vya Afya vinatakiwa kukidhi viwango vya utoaji huduma kwa Wagonjwa; lakini Hospitali nyingi na Vituo vya Afya vingi havina viwango vya utoaji huduma:-

Je, Serikali ina mkakati gani mahsusini wa kuhakikisha Vituo vya Afya na Hospitali vinakidhi viwango vya utoaji huduma.

## **WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

## **178. MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Hospitali ya Mkoa wa Tabora inakabiliwa na changamoto kubwa za Majengo, Wauguzi, Madaktari na Wahudumu wengine wa Hospitali; pia kuna uhaba mkubwa wa vitanda hali inayosababisha Wajawazito kuzalia chini:-

- (a) Je, katika mwaka huu wa fedha Serikali imejipanga vipi kuwasaidia Wananchi wa

Tabora kupata ahueni kwa kutatua kero za Hospitali hiyo inayotegemewa na zaidi ya robo tatu ya wakazi wa Mji wa Tabora;

- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa Wilaya ya Tabora Mjini na Uyuwi nazo zinapata Hospitali.

**179. MHESHIMIWA ZAINABU NUHU MWAMWINDI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Uduavu na utapiamlo ni tatizo kubwa kwa Watoto wengi nchini:-

Je, Serikali ina mpango gani unaotekelzeza wa kukabiliana na hali hiyo ikiwemo kuzijengea uwezo Kamati za Lishe za Kata.

**180. MHESHIMIWA MARIAM NASORO KISANGI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Wapo Watoto wanaoishi Gerezani na huenda Shule na kurudi Gerezani kulala na Mama zao. Hali hiyo sio nzuri kwa malezi ya Mtoto hasa kwa mambo wanayoyaona na kusikia wakiwa Gerezani:-


Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia Watoto hao waondokane na hali hiyo.

### **WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

#### **181. MHESHIMIWA CATHERINE VALENTINE MAGIGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kulinda biashara za wazalishaji wa ndani ili kuwajengea uwezo kuelekea Uchumi wa Viwanda.



### **WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

#### **182. MHESHIMIWA MAFTAHA ABDALLAH NACHUMA (MTWARA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni lini Serikali itavunja Bodi za Wahandisi kutokana na kauli ya Mhe. Rais.

## **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

### **183. MHESHIMIWA GODFREY WILLIAM MGIMWA (KALENGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Jimbo la Kalenga lina vivutio vingi vya utalii vinavyoweza kuingizia Nchi yetu fedha za kigeni kama vile *Isimila Stone Age* na Makumbusho ya Mtwa Mkwawa Mkwavinyika:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa Vijijini kuimarisha na kujenga mazingira na kuvitumia vivutio hivyo ili kuongeza pato la Taifa.

## **WIZARA YA NISHATI:**

### **184. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Mapema mwaka 2016 Waziri wa Nishati alifanya uzinduzi wa mradi wa umeme wa REA na kuagiza Vijiji vya Sarakwa, Tingirima, Rakana, Nyang'aranga, Nyamakumbo, Saba-Oanza, Mmagunga, Nyabuzume, Bukama, Tiring'ati, Bigegu, Nyaburundi, Masaba, Nyansirori, Nyamuswa A, Saloka - Guta, Mahanga, Manchimwero, Nyangere, Makongoro A na B na Nyamuswa kupatiwa umeme:-

- (a) Je, ni nini kifanyike ili miradi ya Vijiji 21 ikamilike kwa wakati kama Serikali ilivyoahidi;
- (b) Je, ni nani aliyepanga Kijiji A kipate Km 3, transforma 2 au nguzo 20 za umeme upitie eneo gani bila kushirikisha Vijiji na hata bila kujali wingi wa Kaya.

#### **WIZARA YA MADINI:**

#### **185. MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI):**

- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-  
Je, ni lini uzalishaji wa Madini ya *Niobium* utanze katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**DODOMA  
07 MEI, 2019**

**S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**